

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA
Namabari ya Simu: +255 026 – 2323267
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya

TAARIFA KWA UMMA
KUWEPO KWA MGONJWA WA CORONA NCHINI TANZANIA

Ndugu Wananchi,

Mnamo tarehe 15 Machi 2020, tulipokea msafiri mtanzania mwanamke mwenye umri miaka 46, ambaye aliwasili na ndege ya Rwandair, akitokea nchini Ubelgiji. Msafiri huyu aliondoka tarehe 3 Machi 2020, ambapo kati ya tarehe 5-13 Machi alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji na kurejea nchini tarehe 15 Machi saa 10 jioni. Msafiri huyu alipita uwanja wa KIA akafanyiwa ukaguzi na kuonekana kutokuwa na homa. Baadae alianza kujisikia vibaya akiwa hotelini na kwenda hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mt. Meru ambapo sampuli ilichukuliwa na kupelekwa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyopo Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi. Vipimo vya maabara vimethibitisha kuwa mtu huyu ana maambukizi ya ugonjwa wa Corona (COVID-19). Mgonjwa anaendelea vizuri na matibabu.

Ninapenda kutumia fursa hii kuwatoa hofu wananchi kwamba Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha ugonjwa huu unadhibiwa ili usisambae nchini. Aidha Serikali inashirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na wadau katika kuendelea kutekeleza mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huu.

Aidha, ninapenda kuendelea kuwataka wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbali mbali. Aidha, kwa kuzingatia **Kanuni ya 46 ya Sheria ya Afya ya Jamii, 2012 (Reg. 46 of the Public Health Regulation (Sanitisation and Hygiene Practices), 2012)**; ninaelekeza mambo yafuatayo:-




Scanned with
CamScanner

UAM

1. Watanzania wasiokuwa na safari za lazima, wanashauri kwa sasa kusitisha safari zao kwenye nchi zenye maambukizi
2. Nazitaka Taasisi zote zikiwemo Shule, Hoteli, Maduka ya Biashara, Nyumba za Kulala Wageni (Lodges/Guest Houses), Mkanisa, Misikiti, Ofisi za Umma na za Binafsi, Vituo vya kutolea Huduma za Afya, taasisi za fedha, vyombo vya Usafiri, pamoja na maeneo ya mikusanyiko ya watu kama vile masoko, viwanja vya mpira, na vituo vya abiria kuweka vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni au maji yenye Klorini kwa ajili ya kuhakikisha usafi wa mikono. Aidha kwa kadri itakavyowezekana, maeneo hayo yawekewe vifaa maalum vya kuwekea vitakasa mikono (*Sanitizer Dispensers*)
3. Kuweka maji yenye dawa ya Klorini au vitakasa mikono (hand sanitizers) katika mageti ya kuingilia hifadhini au mahotelini kwa ajili ya kusafisha mikono ya watalii na waongoza watalii wote.
4. Kuweka maji yenye dawa ya Klorini katika Vituo vya Mabasi ya abiria na Mwendokasi kwa ajili ya kusafisha mikono ya wasafiri.
5. Kuepuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana, kugusa pua, mdomo pamoja na macho kadri itakavyowezekana.
6. Hospitali zetu zihakikishe kuwa ndugu/jamaa wanaokwenda kuona wagonjwa waliolazwa idadi yao isizidi wawili kwa kila mmgonjwa
7. Kutoa taarifa kwenye Ofisi za Afya au Vituo vya Kutolea Huduma za Afya endapo watamwona mtu mwenye dalili za ugonjwa wa COVID-19

Imetolewa na:



Ummy Mwalimu, Mb.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Dae es Salaam.

16/3/2020



Scanned with
CamScanner